# JAWABU LA KCPE 2021
## Darasa la Nane

004

## SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

Muda: Saa 1 dakika 40

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandikia chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala siyo katika kijitabu hiki cha Maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

    NAMBA YAKO YA MTIHANI
    JINA LAKO
    JINA LA SHULE YAKO

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotegwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya majibu na usiikunje
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje
9. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A,B,C,D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    Mfano

    29. Tumia kiambishi sahihi:-
    Darasa __ tajengwa kesho.
    A. i
    B. u
    C. li
    D. ki

Jibu sahihi ni C
Katika karatasi ya majibu

9 [A] [B] [C] [D] 19 [A] [B] [C] [D] 29 [A] [B] [C] [D] 39 [A] [B] [C] [D] 49 [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 29, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

© Booster Education Publishers 2021
P. O. Box 00300-7805, Tel: 0202225440, Cell: 0721819069/0722163391/0722163392
Mombasa Office, Tel: 0721132623
Email: boosterpublishers@yahoo.com

FUNGUA UKURASA



JAWABU

*Kamilisha vihasho nambari 1 - 15 kwa kiteuzi kinachofaa.*

Ushindi ___1___ Kismati ___2___ bahati ambayo ___3___. Alijawa na furaha ___4___ mama aliyejifungua ___5___. ___6___ wake walimpongeza na ___7___ hata akashindwa ashukuru vipi. Wakati ___8___ juu ya jukwaa kuhutubia ___9___ yake, alisindikizwa kwa makofi "___10___!" Ilikuwa siku isiyosahaulika daima.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ulioupata | B. aliyoipata | C. alioupata | D. uliyoipata |
| 2. | A. alikuwa | B. ilikuwa | C. ulikuwa | D. ulikua |
| 3. | A. ni bahati na sibu | | B. hakuilalia hakuiamkia | |
| | C. aliizamia akaizamukia | | D. aliilalia mlango | |
| 4. | A. mithili ya | B. tamthili ya | C. lau | D. halikadhalika |
| 5. | A. aula | B. mapacha | C. sheshe | D. pacha |
| 6. | A. Mashabiki | B. Wapinzani | C. Wachezaji | D. Watazamaji |
| 7. | A. kuizawidi | B. kumzawidi | C. kuzawadi | D. kumzawadi |
| 8. | A. alipopanda | B. akipanda | C. alipanda | D. angepanda |
| 9. | A. halaiki | B. washabiki | C. hudhuria | D. hadhira |
| 10. | A. pa pa pa | B. rap rap rap | C. sa sa sa | D. chwa chwa chwa |

Ushairi ni ___11___ wanafunzi wengi huogopa kwani ___12___ kuwa ___13___ hasa wanapotakikana kubainisha baina ya ___14___; shairi lenye mishororo mitano ni tathlitha. Ila ___15___ akiwa na nia, njia itapatikana.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | A. mada ambayo | B. mada ambao | C. mada ambalo | D. mada ambapo |
| 12. | A. wanafahamu | B. wanajua | C. inaeleweka | D. wana dhana |
| 13. | A. ni ngumu | B. ni mgumu | C. ni gumu | D. ni magumu |
| 14. | A. tathlitha | B. tasdisa | C. takhmisa | D. tathmina |
| 15. | A. anayefunzwa | B. anayefunza | C. anayesoma | D. msomaji |

*Kuanzia swali la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo.*

16. Baba amejenga nyumba moja hapa na nyingine maridadi mjini. Ainisha maneno yaliyopagiwa kistari.
    - A. Kivumishi, kiashiria, kivumishi, kielezi
    - B. Kivumishi, kibadala, kiwakilishi, kielezi
    - C. Kivumishi, kielezi, kivumishi, kivumishi
    - D. Kivumishi, kivumishi, kiwakilishi, kivumishi

17. Chagua sentensi ambayo imetumia kiunganishi kwa usahihi.
    - A. Watoto wanasoma angalau wakicheza.
    - B. Aliadhibiwa bighairi hakukamilisha ziada.
    - C. Walau ya kufeli, alikosa nafasi katika shule.
    - D. Lau ukirauka utamwahi kabla hajaondoka.

18. Ni vifaa gani vya mekoni havikuambatanishwa sawasawa?
    - A. Kinu - mchi
    - B. Chungu - kifunikio
    - C. Sahani - kawa
    - D. Mbuzi - kung'uto

31. Hotuba uliyoisoma ilitolewa:-
   A. asubuhi gwarideni na mwanafunzi mmoja.
   B. wakati wa mtikati na mwanafunzi mmoja.
   C. magharibi na mmoja wa wanafunzi.
   D. gwarideni adhuhuri na mmoja wa wanafunzi.

32. Mwanafunzi ambaye alitoa hotuba hii:-
   A. alikuwa na ustadi kuliko wote katika kuhutubu.
   B. alichaguliwa kuwakilisha wanafunzi kuhutubu.
   C. aliwahi kuathirika na utumiaji wa vileo.
   D. alikuwa na ujuzi wa kufafanua athari za mihadarati kwa mwanfunzi.

33. Mwandishi anaposema kuwa mwangata mbili moja humponyoka, anadhamiria kusema kuwa:-
   A. mradi ujue kusawazisha mambo, haidhuru kuyafanya pamoja
   B. iwapo utatumia vileo ukiwa shuleni, elimu yako itatumbukia nyongo
   C. kwa sababu ya kuepuka mihadarati, wengi wamedunisha alama zao
   D. njia pekee ya kuepuka mihadarati ni kujifunga kibwebwe darasani

34. Didimia dididi kama kibatari chenye mafuta fifi. Eleza tamathali iliyotumika hapa:-
   A. tashbihi
   B. tashihisi
   C. kinaya
   D. sitiari

35. Kuanguka kichwangomba ni:-
   A. kushuka alama zikilinganishwa na za awali
   B. kushindwa na wanafunzi wengi uliowashinda awali
   C. kuanguka kiasi cha kutoa sauti kama kombamwiko
   D. mwanguko wa kichwa chini miguu juu kuashiria matokeo duni

36. Ni gani si njia ya kumtambua mwanafunzi mlevi?
   A. Kubadilika kwa rangi ya kinywa hasa meno.
   B. Kudungwa na miba anapotembea kipopo.
   C. Kuparara kwa mwili ukawa kijivu.
   D. Maozi husharabu wekundu wa damu.

37. Wanafunzi wanaoepuka kuhudhuria masomo shuleni ni wale ambao:-
   A. hawashiki chochote walimu wanapofundisha
   B. wanawaibia wazazi wao kwa kutumia ujanja
   C. wanawania kufisha ndoto zao kuhusu mustakabali
   D. wamekuwa na mazoea ya mihadarati ili waende inakouziwa

38. Mihadarati inaukoseaje ulimwengu hasa?
   A. Kwa kuwafanya wanafunzi waraibu
   B. Kusababisha serikali kugharimika kununua dawa
   C. Kuzidisha idadi ya chokora mijini
   D. Kuwaboronga watu ambao hatimaye wangechukua vyeo vya wale walioacha kazi

39. Asanteni kwa 'kutupiga jeki' mwandishi ana maana kuwa walimu wao:-
   A. wanawaadhibu kila wanapokanyaga chechele
   B. wamewasaidia katika kuwainua masomoni
   C. wanawapa muda wa kuyapima mambo vilivyo
   D. huwatambua watovu wa nidhamu walivyo

40. Mihadarati haiitwi:-
   A. vileo
   B. dawa za kulevya
   C. uraibu
   D. muhadarati

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 - 50.*

Kinyume na wanafunzi wengine darasani waliokuwa wacheshi kama kinyago, Kabeti daima dawamu aliketi pembeni mwa darasa akiwa amejikunyata na kushika tama. Isitoshe alizama katika lindi la mawazo chungu nzima huku macho yake yakionekana machovu. Ni kana kwamba hakuwa akilala, na kama alilala, basi alilala usono wa mang'amung'amu. Siku hiyo mimi pamwe na wasena wangu tuliamua tuende kumuuliza kilichomzamisha katika hali ile ya jitimai na majonzi yaliyodondosha machozi. Licha ya kumdadisi, hakusema lolote wala kutoboa siri yoyote kwani aliamini kuwa hakuna siri ya watu wawili, siri ibaki sirini.

Tulipoona juhudi si pato, tuliamua kuendelea na hamsini zetu. Wengine wakaenda kustawisha soga nasi wengine kucheza kibemasa. Kengele ya kurejea madarasani ilipokirizwa, kama ilivyokuwa desturi, tulifululiza hadi madarasani ila kinyume na kawaida kabeti hakuwapo. Alifanya mambo kisengerenyuma. Tukitoka anabaki, tukirudi, anatoka. "Ni nini kinachomsumbua?" Nilitatizika. Hata Bwana Odoyo mwalimu wa king'eng'e alipoingia akaona Kabeti hayupo, aliulizia na kutoka sawia kuenda kumtafuta.

Kabeti hakupatikana popote, na hilo lilimtia hofu kila aliyemjua. Kumpata nje ya darasa kulikuwa muhali. Kwa hivyo lilikuwapo la mno kwani penye moshi hapakosi moto. Moto upi? Tuliulizana. Mara kikasikika kilio kikali kutoka misala ya wasichana. Walimu na wafanyakazi wa shuleni wakakimbia huko huku sisi tukizuiliwa madarasani.

"Mola wanguuu! Msaidiee! Msaidie tafadhali. Nisingependa aniache pekee katika ulimwengu huu uliojaa mawi. Nitawaleaje maumbu zangu tandatu?" Ilikuwa sauti ya Kibeti. Akilia kama hinziri aliyechinjwa kichikichi. Walimu walimkimbilia. Wakamwahi na kumkumbatia. Uso kalowa machozi chapachapa mtoto. watu kazidiwa na mzongo. Baada ya ushauri nasaha, ndipo alipowaelezea walimu changamoto zilizowakisha moto makaoni mwao. Akaeleza alivyokesha kumtunza mama yake aliyeteswa na maumivu usiku kucha. Alivyohangaika kuwatunza ndugu zake walungizi. Kisha wakishaibwa na usingizi afanye kazi za nyumbani kabla ya kuifanya ziada yake.

Walimu walimsikiliza mioyo ikadondoka huruma. Bila kulimatia, walichangachanga kidogo walichokuwa nacho, jioni iyo hiyo wakaandamana naye kuenda kwao kujionea hali halisi. Naarifiwa walimu walishangaa ni vipi Kabeti alimudu kudumu katika hali ngumu kiasi kile. Wakafanya walichoweza. Mama aliyetelekezwa na mumewe akachukuliwa hospitalini. Nyumba ikapigwa deki nguo zikafuliwa na mazingira kusafishwa, vyombo vilioshwa na chakula maridhawa kununuliwa. Kwa mara ya kwanza, Kabeti akashusha pumzi na kutabasamu. Akaamini chambilecho wahenga kuwa kilio huanza mfiwa...

19. Chagua mahali neno 'karibu' limetumika kuonyesha makisio.
   A. Watoto wanaokaa karibu na dirisha wamelala.
   B. Karibu jiwe limwangukie kuku wangu.
   C. Babu yake ana karibu miaka themanini.
   D. Usiingie kwa mwenyewe kabla ya kukaribishwa.

20. Sentensi, Mwanamke wa <u>ki</u>arabu a<u>ki</u>suka nywele zake <u>ki</u>juso chake huonekana njia ya kuchekesha; imetumiaje kiambishi 'ki'?
   A. Udogo, hali endelezi, udogo
   B. Aina, masharti, udogo
   C. Kielezi, hali endelezi, udogo
   D. Udogo, masharti, udogo

21. Teua pale ambapo pana kielezi miongoni mwa viteuzi ulivyopewa.
   A. Yohana alitaka kuuliza swali lipi?
   B. Ni sherehe gani hiyo utakayoihudhuria?
   C. Watoto wanachezea wapi leo?
   D. Mbona mgonjwa amekataa dawa?

22. Ni sentensi ipi inayoshirikisha kitenzi kilichoradidiwa?
   A. Ni suala hili hili lililoleta balaa na belua.
   B. Kitoto kilikimbiakimbia uwanjani kikicheza.
   C. Harakaharaka haina baraka.
   D. Wimbo mzurimzuri huongoa moyo wa mtu.

23. Wingi sahihi wa sentensi; Ghulamu na binti huyu huishi karibu na soko kule mtaani ni:-
   A. ghulamu na mabinti hawa huishi karibu na masoko kule mitaani.
   B. maghulamu na mabinti hawa huishi karibu na masoko kule mitaani.
   C. waghulamu na mabinti hawa huishi karibu na soko kule mijini.
   D. maghulamu na mabinti hawa huishi karibu na soko kule mtaani.

24. Mwanafunzi ambaye anakufa moyo ni yule ambaye anakuwa na wasiwasi. Iandike sentensi upya bila ya -amba.
   A. Mwanafunzi akufaye moyo ni yule akuwaye na wasiwasi.
   B. Mwanafunzi afaaye moyo ni yule awaye na wasiwasi.
   C. Mwanafunzi anayefa moyo ni yule anayewa na wasiwasi.
   D. Mwanafunzi afaye moyo ni yule awaye na wasiwasi.

25. Ni sentensi gani sahihi kimantiki?
   A. Mchuzi mchuuzi ana mjuzi mtamu.
   B. Mjusi mchuuzi ana mjuzi mtamu.
   C. Mchuuzi mjusi ana mchuzi mtamu.
   D. Mchuuzi mjusi ana mjuzi mtamu.

26. Benta umbu yake Gloria, ameolewa na Kena ambaye ni kaka wa Rhoda. Je, Gloria atamwitaje Rhoda?
   A. Shemeji　　B. Wifi
   C. Mlamu　　D. Mwanyumba

27. Chagua kundi ambalo kitenzi chake hakikunyambuliwa katika hali ya kutendesha.
   A. Ingia - ingisha
   B. Poa - poza
   C. Pona - ponya
   D. Tokota- tokosa

28. Mojawapo si siku ya juma. Ipi?
   A. Juzi　　B. Mtondogoo
   C. Jana　　D. Kitojo

29. Nambari au idadi inayogawika kwa moja au yenyewe huitwa nambari:-
   A. shufwa　　B. tasa
   C. kipeo　　D. witiri

30. Kila mtu au jambo huwa na hitilafu kuonyesha kutokamilika kwake. Ni methali gani haielezei hali hii:-
   A. hakuna chema kikosacho ila
   B. chema hakidumu
   C. mwanamke mwema hakosi kasoro
   D. majumba makubwa husitiri mambo

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40.*

"Mwalimu Mkuu Bwana Suluhu, Naibu Mwalimu Mkuu Bi Kazi, Walimu wetu wapenzi, viranja ajmaina, wanafunzi wenzangu, mabibi na mabwana, masalkheri. Kwanza nishukuru shukrani za dhati kwa fursa hii adimu na adhimu tuliyopata kujumuika hapa. Mnavyofahamu, magwaride sampuli hii hutokea kwa nadra. Lakini ikitokea haja, hatuna budi. Si walisema wa tangu tangu kuwa lisilo budi hutendwa?

Ninasimama kadamnasi, si kwa sababu nina ujuzi wa ajuza. Hasha. Ni kwamba nimeteuliwa kutoa hotuba kuhusu madhara ya mihadarati, hususan kwa mwanafunzi. Sitapoteza muda kueleza maana ya mihadarati maadamu mmekutana nalo mara si moja. Mihadarati ni sumu kwa jamaa na jamii kwa jumla. Hivyo basi mwanafunzi yeyote atakayethubutu kuitumia hatakosa kudhurika pakubwa.

Tukianzia matokeo duni, ni wazi kuwa mwangata mbili, moja humponyoka. Vileo na masomo ni kama Lila na Fila, havitangamani. Bila shaka alama zako zitadidimia dididi kama kibatari chenye mafuta fifi. Hii ni kwa sababu kileo chochote kiwacho huuvuruga ubongo na kumfanya mtumiaji wake kufanya mambo kipopo. Ni nani miongoni mwetu angependa kuanguka kichwangomba? Naamini hakuna hakunani.

Mbali na kudorora kimasomo, siha ya mwanafunzi hupata nyufa. Madhara haya ni jahara kama meno ya ngiri. Wekundu wa damu machoni, meno yaliyobadilika rangi na ngazi iliyozingia. Kwa nini tujichome kwa miiba ilhali tunaona? Tutambue kuwa sana ikizidi sana, dawa hizi za kulevya huweza kuleta maradhi ya kufisha kama saratani, kifuakikuu, ugonjwa wa maini na ndwele nyinginezo. Je, twataka kufa tungali wachanga?

Utoro ni madhara mengine. Aghalabu mwanafunzi mraibu hutafuta mbinu ya kuhepa shule aende kwa mgema. Usisahau kuwa uraibu huo huweza kumsukuma afanye vitendo viovu ili kupata pesa. Mara awatapeli wazazi ama kuiba vitu vya wenzake shuleni akauze bei ya kutupa. Ukiwa mtoro, utatimizaje ndoto yako? Utakuwa na mustakabali gani? Hapa tunao marubani wa kesho na machura vile vile. Ukitaka kuwa ombaomba kesho, zama zi katika bahari ya vileo.

Sitakamilisha bila kusema kuwa wanafunzi tukijitosa kwenye mihadarati, tutaikosesha dunia ya kesho watu muhimu. Watu watakaochukua nafasi za uongozi wazee waking'atuka na kustaafu. Ina maana kuwa hata taifa la kesho litakuwa hatarini tusipojihadhari leo. Wanafunzi wapendwa. Ningesema mengi lakini muda hauruhusu. Naomba tuende tutafakari haya machache niliyofafanua. Tukikutana tena Inshallah, tutanoana zaidi. Asanteni walimu kwa kutupiga jeki na kutushika mkono hasa tunapokanyaga chechele. Tunaahidi kufuata nyayo zenu kwani penye wazee hapaharibiki neno. Jalali awabariki na muwe na siku njema nyote. Asanteni."

41. Teua kauli hapa isiyoambatana na aya ya kwanza:-
A. kule alikoketi darasani, Kabeti hakuwa akisoma.
B. Kabeti alidhurika kwa kutopata muda wa kulala.
C. mawazo yaliyomtatiza Kabeti hayakuhusu masomo.
D. wanafunzi wengi darasani walikosa furaha.

42. Kabeti alitaka siri yake isijulikane na yeyote kwa sababu:-
A. alikosa nguvu na ujasiri wa kutoboa siri hiyo
B. wengi tayari walifahamu siri yenyewe
C. alikuwa msiri kama usiku
D. kawaida watu wakijua siri ya mtu hawaitunzi

43. Mchezo alioshiriki mwandishi na wenzake ni ule wa:-
A. kurusha vijiwe kweye mashimo
B. kukisia kilichofumbatwa mkononi
C. kujificha na kutafutana
D. kushikana, kumenyana na kuangushana

44. Kauli ya kweli kuhusiana na Bwana Odoyo ni kwamba:-
A. alifundisha Kiswahili akijua Kabeti hayupo
B. alifundisha somo la Kiingereza
C. alifunza kabla ya kutambua asiyekuwamo
D. alimwendea Kabeti punde baada ya kipindi

45. Kwa kawaida Kabeti:-
A. alikuwa mzoefu wa kusalia darasani
B. alishika tama alipocheza na wenzake
C. alizoea ucheshi kama wengine darasani
D. alitoweka kama jini na kutokea ghafla

46. Mzongo wa mawazo uliomtinga Kabeti ulibainika bayana wakati ambao:-
A. aliangua kilio akijisemeza kwa ukwezi
B. alipotea kutoka darasani kila alipozidiwa
C. alitafutwa kila mahali kama moshi wa moto
D. alikataa kulifichua lililomla kichwa

47. Kwa kawaida Kabeti alipowasili kiamboni kutoka shuleni:-
A. alianza kwa kukamilisha ziada yake
B. aliwagawia ndugu zake kazi wakasaidiana
C. alijishughulisha na majukumu mengi ya baitini
D. alianza kwa kumtunza mama yake mpendwa

48. Hatua ya walimu baada ya kujua hali halisi ya Kabeti inadhihirisha methali zote hizi ila:-
A. Kutoa ni moyo, usambe ni utajiri
B. Heri jirani karibu kuliko ndugu mbali
C. Penye miti hapana wajenzi
D. Niazikiwa moja, kilicho mbali huja

49. Ni kauli ipi isiyokuwa kweli kuhusiana na mama yake Kabeti?
A. Hatimaye alifuata njia ya marahaba.
B. Mume wake hakuweza kumudu tiba yake.
C. Alikuwa mgonjwa kwa kipindi kirefu.
D. Mume wake alikuwa amemwacha.

50. Kamilisha methali katika sentensi ya mwisho ya kifungu:-
A. maana mwenye uchungu ndiye
B. kwani ndiye mwenye uchungu
C. ndipo wa mbali wakaja
D. akafuatia mfu